# WACHUNGAJI WATANGULIZI NCHINI TANZANIA

*Re-aranged and translated by Pastor Stephen Letta*

**Salimu Justin Kimera, (1904–1980)**

Salimu Justin Kimera alikuwa mkurugenzi mzawa wa kwanza wa Misheni ya Tanganyika Mashariki.

**KUZALIWA**

Salimu Justin Kimera alizaliwa Bumbuli mwaka 1904, kwenye milima ya Usambara, wakati wamishionari wa Kiadventista walipokuwa wamefika Tanganyika. Mama yake alijulikana kama Kivunga, lakini hakuna mengi yanayojulikana kuhusu baba yake. Salimu alikulia katika familia ya kawaida ya Kiislamu na hivyo katika utoto wake alisoma madrassa (shule ya Kiislamu). Alikuwa na shauku kubwa ya elimu rasmi hivi kwamba alitoroka nyumbani na kutafuta shule. Alikwenda Mkomazi ambako alikutana na Petro Risase Kime ambaye alimpeleka Kihurio Mission School ambako alitimiza ndoto yake ya kupata elimu.

**MAFUNZO YA UALIMU**

Baada ya kupata elimu ya msingi, alipata mafunzo ya ualimu katika Chuo cha Ualimu cha Suji. Mapema miaka ya 1940, yeye na Ezekiel Mafuru walibahatika kupata mafunzo ya Kiingereza na afya huko Malamulo nchini Malawi. Walimu hawa wawili tu ndiyo waliochaguliwa kutoka Tanganyika. Hii ilifanyika kwa makusudi ili kuanzisha Kiingereza kama somo katika shule za Waadventista. Hilo lilimfanya kuwa mhimizaji wa Kiingereza kutumika kama somo la kujifunza mashuleni na mtetezi wa maisha yenye afya. Kimera alifundisha katika shule kadhaa tofauti, lakini hasa shule za Ikizu, Kibumaye, Utimbaru, Busegwe, na Suji. Pia aliwahi kuwa mkurugenzi wa shule za kanisa katika eneo la Mara.

**MAFUNZO YA UCHUNGAJI**

Pia alikuwa amepata mafunzo ya uchungaji, kwa hiyo akawa mchungaji na kutumika sehemu kadhaa. Hizi ni pamoja na Mbeya, Tukuyu, Iringa, Moshi, na Tanga, miongoni mwa nyinginezo. Alifanya kazi pia kama mkurugenzi katika Misheni ya Pare. Alikuwa Mwafrika wa kwanza kuongoza misheni kati ya 1957 na 1960. Hii ilikuwa kabla ya misheni hiyo kuwa Fildi Misheni ya Tanganyika Mashariki. Alikuwa mmoja wa wachungaji wachache kutoka jamii ya kabila la Wasambaa.

**KUFUNGA NDOA**

Mchungaji Salimu Justin Kimera alifunga ndoa na Kompeho Mose na walipata watoto 12 ambapo watatu walifariki wakiwa wachanga. Wale tisa waliosalia ni pamoja na wavulana watatu na wasichana sita.

**KUSTAAFU**

Mchungaji Kimera alistaafu kutoka kwa huduma hai mwanzoni mwa miaka ya 1970. Baada ya kustaafu aliendelea na shauku yake ya utume, akifungua makanisa katika

maeneo ambayo hayajafikiwa na injili. Mchungaji Kimera alikuwa anaweza kutembea zaidi ya maili kumi kwa miguu ili kupeleka ujumbe maeneo mapya. Kazi hiyo aliifungua Korogwe ambako sasa kuna mitaa yenye makanisa zaidi ya kumi. Salimu Justin Kimera alifariki Desemba 14, 1980.